TANGAZO LA SERIKALI Na. 1023 La Tarehe 11/12/2020

(SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya Kiteto za Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakavyoelekezwa vinginevyo;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa dawa, hii ni pamoja na: -

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;

(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula; au

(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto;

*Tangazo la Serikali Na. 1023 (Linaendelea.)*

"kaya" maana yake ni familia inayojumuisha baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"maji taka" maana yake ni kinyesi au mkojo na uchafu mwingine kama maji ya kuoga na maji ya kupigia deki, kuosha vyombo, maji yanayotokana na uchafu kutoka vituo vya mafuta, vituo vya kuoshea magari na viwandani ambapo yana kemikali au yasiyokuwa na kemikali na ambayo hayajasafishwa;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri au anafanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

3.- (1) Kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake.

(2) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanja au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mifereji ya kupitisha maji inayozunguka au kupita kando ya nyumba, kiwanja au eneo la biashara yake.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha

(1), na cha (2) kila mkazi atakuwa na wajibu wa kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika kila jumamosi ya mwisho wa mwezi au katika siku itakayopangwa na Halmashauri.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu atakuwa ametenda kosa.

Uwekaji taa za nje ya nyumba na upakaji rangi

4. (1) Kila mmiliki wa nyumba au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli za biashara na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.

(2) Mtu yeyote ambaye, bila sababu za msingi atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu

5. (1) Mmiliki wa nyumba, kiwanja au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa katika eneo lake hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

(2) Mtu yeyote ambaye bila sababu za msingi, atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Upulizaji dawa

6. (1) Mtu yeyote anayeendesha biashara ya upuliziaji dawa ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni hai kutoka Halmashauri;

(b) kusimamiwa na Afisa Afya wakati wa upulizaji; na

(c) kutoa cheti baada ya kupuliza dawa kilichosainiwa na Afisa afya.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Matengenezo na maegesho ya magari, pikipiki na mitambo

7. (1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Mtu yeyote:

(a) hatoruhusiwa kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo; au

(b) kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi au barabarani.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka, bila sababu za msingi, masharti ya kifungu kidogo cha (2) atakuwa ametenda kosa.

.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula.

8.- (1) Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kutimiza masharti na kanuni za afya; na

(b) kuwa na kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka, bila sababu za msingi, masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Machinjio na maduka ya nyama

9. (1) Mtu yeyote hatoruhusiwa:

(a) kwa madhumuni ya kibiashara kuchinja mifugo katika maeneo yasiyokuwa machinjio;

(b) kuuza nyama ya aina yoyote katika

maeneo yasiyokuwa maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(c) kuuza nyama isiyokaguliwa na mtaalamu wa mifugo au mtaalamu wa afya; na

(d) kusafirisha nyama kwa madhumuni ya kibiashara toka machinjioni bila kutumia gari maalumu la kusafirishia nyama lililoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama atatakiwa kuhakikisha yafuatayo:

(a) duka lake ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi sita kutoka usawa wa sakafu;

(b) duka lake lina maji safi, misumeno ya kukatia nyama na vyuma vya kutundikia nyama;

(c) duka lake lina kabati la vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na mizani ya kupimia nyama;

(d) duka lake lina pipa au kifaa cha kuhifadhia takataka;

(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe na kofia nyeupe;

(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita; na

(g) duka lake lina karo la maji machafu.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa biashara ya hoteli na hosteli

10. (1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni, hosteli, shule, kituo cha kutolea huduma za afya au nyumba ya biashara kabla ya kuanza biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha:

(a) jengo lake limekaguliwa na Afisa Afya; na

(b) amepata kibali cha Halmashauri cha

kufanya shughuli husika.

(2) Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, hosteli, shule, kituo cha kutolea huduma za afya au nyumba ya biashara kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa mahitaji yafuatayo yamezingatiwa: -

(a) jengo lina mwanga na hewa ya kutosha;
(b) jengo lina nafasi na vifaa vya kutosha;
(c) uimara wa jengo;
(d) jengo lina mfumo imara wa uondoshaji wa maji taka, miminika na taka ngumu;
(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;
(f) jengo lina vyoo na mabafu ya kutosha kwa jinsia zote;
(g) jengo lina vifaa vya zima moto;
(h) tanki la kuhifadhia maji safi;
(i) vyoo na bafu vimesakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita toka usawa wa sakafu;
(j) kwa nyumba za kulala wageni na hosteli, uwepo wa vyandarua.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (3), wakati wowote Halmashauri ikijiridhisha kuwa mmiliki hajakidhi masharti ya afya inaweza kuzuia utoaji wa huduma husika mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti ya kiafya yaliyotolewa na Halmashauri.

Ukaguzi wa afya.

11. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya kabla ya kutoa au kuhuisha leseni ya biashara.

Eneo la kutupa taka

12. (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa: -

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;

(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na

(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

(2) Mtu yeyote atakayetupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, uchochoro, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo atakuwa ametenda kosa.

Vikundi vya wazoa taka

13. Halmashauri itahamasisha uundaji wa vikundi jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Magari ya abiria kuwa na vyombo vya kuhifadhia takataka

14. (1) Kila mmiliki wa gari la abiria litakaloingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka kwenye chombo hicho.

(2) Endapo abiria atatupa takataka nje ya chombo cha usafiri, mmiliki au dereva au kondakta atachukuliwa kuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushtakiwa mahakamani chini ya Sheria Ndogo hizi.

Uhifadhi maji taka

15. (1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa: -

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;

(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Ada ya utozaji taka

16. (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kila mwezi kutoka kwa kila kaya, wamilliki wa nyumba za biashara, taasisi na kampuni zilizopo ndani ya eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Endapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo, Halmashauri itamtaka kulipa deni hilo na adhabu ya asilimia hamsini ya ada anayostahili kulipa.

(4) Endapo mzalishaji taka atashindwa, bila sababu za msingi, kulipa gharama ya huduma kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

17. Kila mmiliki wa jengo la makazi au la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba jengo lake lina choo safi, imara na madhubuti na kuhakikisha kuwa kinatumika wakati wote.

Vyoo vya umma

18. Halmashauri inaweza kujenga vyoo vya umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma vitakavyotoa huduma kwa malipo katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

Vyoo vya muda katika mkusanyiko

19. (1) Mtu, kikundi au taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa muda maalum katika eneo ambalo halina choo cha kudumu itatakiwa kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.

(2) Mtu, kikundi au taasisi itakayokiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa imetenda kosa.

Ilani ya kujenga choo

20. (1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

(2) Mmiliki wa nyumba atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Ilani iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.

Ilani ya kuondoa kero

21. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa makazi au biashara

hadi hapo hali itakapokuwa imerekebishwa.

(3) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Upimaji wa afya

22 (1) Kila mmiliki wa sehemu inayotoa huduma ya hoteli, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili kuuza atatakiwa kuhakikisha kuwa wahudumu wake wanapima afya kila baada ya miezi sita na kulipa ada ya upimaji wa afya kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mmiliki yeyote atakayekiuka mashartiya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uteuzi wa wakala

23. Mkurugenzi anaweza kuteua kampuni, kikundi au mtu binafsi kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

24 Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hizi atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote viwili kwa pamoja.

Kufililisha kosa

25. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo Tangazo la Serikali Na. 238 la tarehe 24.10.2008

26. Sheria Ndogo hizi inafuta Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa mazingira ya Wilaya ya Kiteto, za Mwaka 2008.

______

JEDWALI LA KWANZA

______

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SEHEMU YA I
ADA YA UZOAJI TAKA

| | AINA YA JENGO AU -BIASHARA | ADA KWA MWEZI |
|---|---|---|
| 1. | Eneo la makazi kwa kaya | 2,000/= |
| 2. | Chumba cha kuuzia chai | 2,500/= |
| 3. | Mgahawa | 3,000/= |
| 4. | Wauza barafu | 2,500/= |
| 5. | Mgahawa mkubwa | 5,000/= |
| 6. | Nyumba za kulala wageni | 10,000/= |
| 7. | Zahanati binafsi | 5,000/= |
| 8. | Vituo vya afya (binafsi) | 7,500/= |
| 9. | Hospital (binafsi) | 10,000/= |
| 10. | Viwanda vidogo au garage | 5,000/= |
| 11. | Hoteli: Vyumba 1-10 | 20,000/= |
| | Vyumba 11-20 | 40,000= |
| | Vyumba 21-30 | 45,000= |
| | Vyumba 31-40 | 60,000/= |
| | Vyumba 41-50 | 70,000/= |
| | Vyumba 51-60 | 80,000/= |
| | Vyumba 61-70 | 90,000/= |
| | Vyumba 71- na zaidi | 100,000/= |
| 12 | Fundi seremala/karakana/kuchoma vyuma | 5,000/= |
| 13. | Maduka ya jumla | 12,000/= |
| 14 | Duka rejareja | 6,000/= |
| 15. | Shule ya msingi(binafsi) | 7,500/= |
| 16. | Vyuo binafsi | 6,500/= |
| 17 | Shule za Sekondari (binafsi) | 10,000/= |
| 18. | Local brewer(legal authorized) | 3,000/= |
| 19. | Bar | 10,000/= |
| 20. | Meza za matunda | 2,500/= |
| 21. | Mama Lishe au Baba Lishe | 3,000/= |
| 22. | Bucha | 4,500/= |
| 23. | Duka la dawa | 6,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 1023 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 24 | Maduka makubwa ya dawa(phamarcy) | 8,000/= |
| 25. | Waosha magari | 6,000/= |
| 26. | Godowns | 8,000/= |
| 27. | Maduka ya vipuri | 6,000/= |
| 28. | Kuuza magazeti | 1,000/= |
| 29. | Makanisa | 5,000/= |
| 30. | Misikiti | 5,000/= |
| 31. | Wasusi | 3,500/= |
| 32. | Vinyozi | 4,500/= |
| 33. | Wauza mkaa | 5,000/= |
| 34. | Fundi cherehani | 2,500/= |
| 35. | Duka la vifaa vya ujenzi | 15,000/= |
| 36. | Maduka ya nguo | 7,500/= |
| 37. | Maduka ya vitabu | 15,000= |
| 38. | stationary | 10,000/= |
| 39. | Wauza mbao | 5,000/= |
| 40. | Mashine za kusaga na kukoboa | 7,500/= |
| 41. | 0fisi za watalii na usafirishaji | 15,000/= |
| 42. | Vituo vya mafuta(petrol station) | 10,000/= |
| 43. | Supermarket (ndogo) | 10,000/= |
| 44. | Supermarket (kubwa) | 75,000/= |
| 45. | Kufyatua matofali | 5,000/= |
| 46. | Duka la kubadilisha fedha | 7,500/= |
| 47. | Ofisi ya watumishi (1-10)<br>0fisi ya watumishi (11-20)<br>Ofisi ya watumishi (21-50)<br>Ofisi ya watumishi (51-na zaidi) | 2,000/=<br>3,500/=<br>4,500/=<br>7,500/= |
| 48. | Night club | 10,000/= |
| 49. | Vituo vya kuuzia maji (water kiosk) | 1,000/= |
| 50. | Computer service | 5,000/= |
| 51. | Dobi | 3,000/= |
| 52. | Maabara (laboratories) | 10,000/= |
| 53. | Wachoraji | 2,000/= |
| 54. | Bakeries (maduka ya kuuzia mikate) | 8,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 55. | Studio | 4,000/= |
| 56. | Stores | 5,000/= |
| 57. | Viwanda (taka nzito kwa tani) | 5,000/= |
| 58. | Viwanda (taka nyepesi kwa trip)<br>Hospitali<br>Vitanda (1-10)<br>Vitanda(11-20)<br>Vitanda (21-30)<br>Vitanda (31-40)<br>Vitanda(41-50)<br>Vitanda (51-60<br>Vitanda (61-70)<br>Vitanda (71-80)<br>Vitanda (81-90)<br>Vitanda (91na zaidi) | 20,000/=<br><br>10,000/=<br>12,000/=<br>20,000/=<br>30,000/=<br>40,000/=<br>50,000/=<br>60,000/=<br>70,000/=<br>90,000/=<br>100,000/= |

SEHEMU YA PILI

ADA YA UNYONYAJI MAJITAKA

| Na | AINA YA BIASHARA | KIASI KWA SAFARI MOJA (TRIP) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi | 35,000/= |
| 2. | Taasisi | 50,000/= |
| 3. | Viwanda | 100,000/= |
| 4. | Kukodi gari nje ya Wilaya | 500,000/= kwa siku bila gharama za mafuta |

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 22(1))*

ADA YA UPIMAJI AFYA

| Aina ya Biashara | Ada kwa miezi |
|---|---|
| kila mhudumu wa hoteli,mgahawa,baa,bucha,sehemu za kuoke mikate,nyumba za kulala wageni,grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili kuuza kupima afya kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya na kujisajili kwa Halmashauri ili kubainisha usalama wa afya yake kabla ya kutoa huduma kwa wateja kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Afya ya Jamii namba 1 ya mwaka 2009 .Kila mhudumu atapimwa afya yake kila baada ya miezi sita(6) | 18,000/= kila anapopimwa |

*Tangazo la Serikali Na. 1023 (Linaendelea.)*

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 25)*

HATI KUFILILISHA KOSA

Mimi……………………………………………………..………. nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto/Afisa mwidhiniwa kwa niaba ya Mkurugenzi, kwamba Tarehe ………Mwezi………. Mwaka………. nilikutwa na kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto za Mwaka 2020, nipo tayari kulipa kiasi cha shilingi…………………na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu

Leo Tarehe……………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...

Cheo…………………………………….

Saini………………………………………

Tarehe……………………………………

Nembo ya Halmashgauri ya Wilaya ya Kiteto imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 16/4/2020 mbele ya:-

TAMIM H. KAMBONA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Kiteto*

LAIRUMBE MOLLEL,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Kiteto*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*